# OFISI YA RAIS
# TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA
# HALMASHAURI YA WILAYA YA BUNDA

SHULE YA SEKONDARI CHITENGULE,
S. L. P 29,
**BUNDA.**

**Kumb. No. CSS/AV/JI/VOL1/17** **11.12.2020**

**Ndugu**

________________________________________

WA ................................................................................................

**YAH: KUCHAGULIWA KUJIUNGA NA KIDATO CHA KWANZA KATIKA SHULE YA SEKONDARI CHITENGULE MWAKA WA MASOMO 2021.**

## 1.0 UTANGULIZI

Ninafurahi kukuarifu kuwa umechaguliwa kujiunga na kidato cha kwanza katika shule ya Sekondari Chitengule mwaka 2021. Shule ipo umbali wa kilometa 2 kutoka Kibara Senta, kwenye barabara ielekeayo Mumagunga, Halmashauri ya wilaya ya Bunda.

Muhula wa kuanza masomo utaanza Tarehe 11/01/2021 unatakiwa kuripoti shuleni kuanzia tarehe **11/01/2021** na mwisho wa kuripoti ni tarehe **25/01/2021**. **Unasisitizwa** kuripoti ndani ya muda uliopangwa, usiporipoti ndani ya muda uliopangwa hautapokelewa na nafasi yako itachukuliwa na mwanafunzi mwingine.

## 2.0 MAMBO MUHIMU YA KUZINGATIA

### 2.1 SARE YA SHULE

(i) Shati mbili (2) nyeupe mikono mifupi (Tetroni) zisizobana (wavulana na wasichana)

(ii) Suruali mbili (2) rangi ya damu ya mzee zenye Marinda mawili kila upande, **zisizobana na ziwe za heshima** (kwa wavulana tu).

(iii) Sketi mbili (2) rangi ya damu ya mzee michirizi miwili myeupe mbele, malinda upana nchi tatu na **urefu iguse viatu** (wasichana tu)

(iv) Viatu vya ngozi visivyo na visigino virefu, sore kubwa na visiwe na urembo wa aina yeyote na **vyenye kamba** (Wavulana na wasichana).

(v) Soksi nyeupe jozi mbili (stocking kwa wasichana) na jozi mbili nyeusi za kawaida kwa wavulana.

(vi) Wasichana waisilamu wanaruhusiwa kuvaa **HIJABU** muhimu iwe ni ndefu.

(vii) Sweta kwa ajili ~~ya~~ baridi rangi ya bluu iliyoiva (Wote)

(viii) Raba kwa ajili ya michezo (wavulana na wasichana)

(ix) Nguo za michezo kwa ajili ya wavulana ni Bukta nyekundu na T-shirt ya bluu, Wasichana Sketi ya njano na T-shirt ya bluu.

(x) Tai rangi ya damu ya mzee.

***N.B : KANDAMBILI NA YEBOYEBO haziruhusiwi kuvaliwa shuleni***

## 2.2 MAHITAJI YA KITAALUMA

(i) Madaftari makubwa kumi (10)

(ii) Kalamu za wino na penseli za kutosha

(iii) Mathematical set (BOFA) moja.

(iv) Faili moja la kutunzia kumbukumbu zako (Aje nalo siku ya kuripoti)

(v) Dictionary kwa ajili ya kujifunzia Lugha ya kingereza

## 3.0 SHERIA NA KANUNI MUHIMU ZA SHULE.

Shule inaendeshwa kwa mujibu wa sheria ya Elimu Na. 25 ya mwaka 1978 na kama ilivyorekebishwa kwa sheria Na. 10 ya mwaka 1995. Aidha shule inazingatia miongozo yote inayotolewa na wizara ya Elimu, sayansi na teknolojia, yenye dhamana ya Elimu nchini na Ofisi ya Rais TAMISEMI yenye jukumu la usimamizi na uendeshaji Elimu. Unatakiwa kuzingatia mambo haya ya msingi:-

(a) Heshima kwa viongozi, wazazi, wafanyakazi wote, wanafunzi wengine na jamii kwa ujumla ni jambo la lazima.

(b) Mahudhurio mazuri katika kila shughuli ndani na nje ya shule kulingana na ratiba ya shule ni lazima.

(c) Kuwahi katika kila shughuli za shule na nyingine utakazopewa.

(d) Kufahamu mipaka ya shule na kuzingatia kikamilifu maelekezo juu ya kuwepo ndani na nje ya mipaka hiyo wakati wote wa uanafunzi wako katika shule hii.

(e) Kutunza usafi wa mwili, mavazi na mazingira ya shule.

(f) Kuvaa sare ya shule wakati wote unapotakiwa

(g) Kuzingatia ratiba ya shule wakati wote.

(h) Kutunza mali ya umma.

**3.1** Makosa ambayo mwanafunzi akiyatenda iwe kwa kujua/kutokujua **atasimishwa** au **atafukuzwa** shule mara moja ni haya yafuatayo:-

(i). Wizi

(ii) Uasherati na ushoga

(iii) Ubakaji

(iv) Ulevi na utumiaji wa madawa ya kulevya kama vile ; uvutaji bangi, cocaine, mirungi, kubeli nk.

(v) Kupiga au kupigana

(vi) Kuharibu kwa makusudi mali ya umma.

(vii) kudharau Bendera ya Taifa.

(viii) Kuoa au kuolewa.

(ix). Kupata mimba au kusababisha mimba ndani na nje ya shule.

(xi) Kugoma, kuchochea na kuongoza au kushiriki kuvuruga amani na usalama shuleni au watu.

(xii) Kukataa kwa makusudi adhabu aliyopewa na kiranja, mwalimu au Mkuu wa shule.

(xiii) Kupatikana na simu ya mkononi shuleni.

**4.0** Mambo mengine muhimu yanayopaswa kukamilishwa na mwanafunzi shuleni.

(i) Fomu ya upimaji wa afya (Medical Examination Form) ambayo itajazwa na mganga Mkuu wa Hospitali ya Serikali.

(ii) Fomu ya maelezo binafsi kuhisu historia ya mwanafunzi na mkataba wa kutoshiriki katika migomo, fujo na makosa ya jinai (iletwe shuleni siku ya kuripoti).

(iii) Fomu ya mzazi kukiri kukubaliana na sheria, kanuni na maelekezo mengine yatakayotolewa na shule. (Iletwe shuleni siku ya kuripoti).

**Tafadhali soma kwa makini maelekezo/ maagizo haya na kuyatekeleza kikamilifu.**

**" KUMBUKA LUGHA YA MAWASILIANO SHULENI NI KINGEREZA"**

**KARIBU SANA KATIKA SHULE HII**

......................................

**CHARLES SOMBA ROBERT**
**MKUU WA SHULE**

MKUU WA SHULE
SHULE YA SEKONDARI CHITENGUL.
S.L.P 29 BUNDA

**NAKALA:**

Mkurugenzi Mtendaji (W)
Halmashuri ya Wilaya ya Bunda
S.L.P 126,
**BUNDA.**

Mkaguzi Mkuu wa Shule (W),
S.L.P ...............
**BUNDA.**

Afisa Elimu (M),
Mkoa wa Mara,
S.L.P 643,
**MUSOMA.**

Mkaguzi wa Shule (Kanda ya Ziwa)
S.L.P 2419,
**MWANZA.**

## FORM FOR MEDICAL EXAMINATION

**PART A:**

**TO THE MEDICAL OFFICER**

Please examine the person below as to his/her physical and mental fitness for enrollment as student, the examination should include the following categories

..............................................................................................................................(Name in full)

(i). Eye-sight
(ii) Hearing
(iii) Limbs
(iv) Speech
(v) Venereal diseases
(vi) Epilepsy
(vii) Neuroses
(viii) Other serious diseases
(ix) Pregnancy

**PART B:**

**MEDICAL CERTIFICATE**

(To be completed by a government medical officer)

(i). Eye-sight ..............................................................................................................................
(ii) Hearing..............................................................................................................................
(iii) Limbs ..............................................................................................................................
(iv) Speech ..............................................................................................................................
(v) Venereal diseases ..............................................................................................................
(vi) Epilepsy ..............................................................................................................................
(vii) Neuroses ..............................................................................................................................
(viii) Other serious diseases ....................................................................................................
(ix) Pregnancy..............................................................................................................................

I have examined the above named person and consider that he/she is/ is not physically and mentally fit for Secondary education studies.

Date ............................ Name ..................................................................Signature ........................

Station .................................... Designation ........................................ Official stamp ........................

[signature]

.....................................................................

**CHARLES SOMBA ROBERT**

**HEADMASTER**

MKUU WA SHULE
SHULE YA SEKONDARI CHITENGULI
S.L.P 29 BUNDA

# SHULE YA SEKONDARI CHITENGULE
# AHADI/KIAPO CHA MZAZI NA MWANAFUNZI

**SEHEMU A: (IJAZWE NA MWANAFUNZI MWENYEWE)**

Mimi ................................................................................ nakubali bila kushurutishwa kuchukua nafasi niliyopewa na Taifa kujiunga na kidato cha kwanza katika shule ya sekondari Chitengule, Ninaahidi kutii sheria na taratibu zote za shule na kwamba nitajituma kujiendeleza kielimu kadri ya uwezo wangu chini ya uongozi wa walezi wangu hapa shuleni. Ninatambua kabisa kutenda kosa ikiwa ni pamoja na kushiriki migomo au kusababisha uvunjifu wa amani shuleni ni kinyume kabisa na sheria na taratibu hivyo naomba uongozi wa shule unichukulie hatua kali za kinidhamu. Ninaahidi kuwa nitahudhuria shuleni muda wote bila kukosa kipindi hata kimoja bila sababu, **EE MUNGU NISAIDIE**

Tarehe ..................................  Sahihi ..................................

**SEHEMU B: (IJAZWE NA MZAZI/MLEZI MWENYEWE)**

Mimi ................................................................................ (jina la mzazi/mlezi). Wa (anwani)........................................................................ ambaye ni ............................(uhusiano na mwanafunzi) wa mwanafunzi........................................................................................ wa sekondari ya Chitengule ambapo motto wangu amechaguliwa kujiunga na masomo ya elimu ya sekondari kidato cha kwanza. Ninaahidi kumpatia mahitaji yote yaliyoagizwa na shule na kwamba nitamuhimiza motto wangu kufuata sheria na kanuni zote za shule.

Tarehe ........................................  Sahihi ....................................

**NB: Fomu hii isijazwe na mtu yeyote ikiwa wazazi wa mwanafunzi wapo hai, isipokuwa tu kama hawapo hai italazimika ijazwe na mlezi anayeishi na mwanafunzi.**